SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la
# RELI NA MATUKIO

Toleo namba 29, Mei 2023

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

# WIZARA YAPITISHIWA TRILIONI 1.113 KUENDELEZA SGR
**Uk. 2 - 3**






## UFAFANUZI KUHUSU KUCHELEWA KUANZA HUDUMA ZA SGR KWA KUTUMIA TRENI YA UMEME
**Uk. 4**



# WIZARA YAPITISHIWA TRILIONI 1.113 KUENDELEZA SGR



**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania – TRC kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imepitishiwa Shilingi Trilioni 1.113 katika bajeti ya fedha ya mwaka 2023/24 kugharamia ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa – SGR, ununuzi wa injini na mabehewa ya mizigo na abiria na upembuzi yakinifu kwa ajili ya miradi ya reli jijini Dodoma, Mei 2023.

Bunge limeidhinisha kiasi hiko cha pesa kwaajili ya kukamilisha ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) na Morogoro - Makutupora (km 422), kuendelea na ujenzi wa njia ya reli ya SGR kwa kipande cha Mwanza – Isaka (km 341), Makutupora – Tabora (km 368); Tabora – Isaka (km 165); na Tabora – Kigoma (km 506), kuendelea na ujenzi wa reli ya Uvinza - Musongati-Gitega (km 282) na taratibu za upatikanaji wa fedha za ujenzi wa reli ya SGR sehemu za Kaliua – Mpanda - Karema (km 321) na Isaka - Rusumo (km 371), kuendelea na ununuzi wa injini, mabehewa na mitambo kwa ajili ya matengenezo ya njia ya reli ya SGR, kugharamia uendeshaji wa reli ya SGR,

Kazi nyingine zilizoainishwa ni pamoja na kuendelea kuwezesha mafunzo ya wataalamu wa uendeshaji na usimamizi wa treni ya SGR, ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa reli, uendelea na uratibu wa utekelezaji wa shughuli za utunzaji wa mazingira na jamii katika utekelezaji wa ujenzi wa reli ya SGR na kuendelea na taratibu za kutafuta mwekezaji kwa ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) kwa mradi wa reli ya Mtwara – Mbambabay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma na Tanga – Arusha – Musoma.

Waziri Mbarawa ameeleza pia kuhusu Mfuko wa Reli (Railway Infrastructure Fund) ambao unasimamiwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuwa unatarajia kutumia jumla ya Shilingi bilioni 294.80 fedha za ndani ili kugharamia ukarabati wa miundombinu ya reli iliyopo na kujenga reli ya SGR, ukarabati wa vitendea kazi na kugharamia maandalizi ya miradi ya ujenzi wa reli.

Kazi zitakazofanyika kupitia fedha za mfuko wa reli ni pamoja na Ukarabati wa njia ya reli ya Kaliua-Mpanda (km 210), Tabora – Kigoma (km 411), na Tabora – Isaka – Mwanza (km 385), Ujenzi wa njia ya reli ya Kilometa 6.2 na daraja kati ya Godegode – Gulwe (km 345 – Km 355), Matengenezo ya njia ya reli ya Tanga - Arusha (Km 470) na Kilosa – Gulwe (km 100), Ufufuaji wa njia za reli zilizofungwa za Kilosa - Kidatu (Km 108) na Manyoni-Singida (km 115), Ukarabati wa karakana, stesheni na majengo ya reli, Ukarabati wa mfumo wa ishara na mawasiliano wa reli iliyopo, Ununuzi wa vipuri kwa ajili ya ukarabati wa mabehewa 600 ya mizigo na mabehewa 37 ya abiria, Ununuzi wa mabehewa 245 ya mizigo, mabehewa 22 ya abiria na injini 10 kwa ajili ya reli iliyopo, Upimaji na uwekaji alama katika maeneo ya reli nchi nzima, Ufufuaji wa Mgodi wa kuzalisha Kokoto wa Pangani (Tanga) na uboreshaji wa Mgodi wa Tura, Ukarabati wa kiwanda cha unyooshaji wa mataruma ya reli (Pugu Sleeper Reconditioning Plant) uliopo Pugu – Dar es Salaam, Ulipaji wa madeni ya watoa huduma, na Uandaaji wa Mpango Kabambe wa Reli (Railway Master Plan).

Kwa upande wa reli iliyopo Bunge limeidhinisha kiasi cha Shilingi bilioni 11.72 kwaajili ya uboreshaji wa reli ya kati kwa kuhusisha uboreshaji wa vituo vya kuhudumia mizigo vya Ilala na Isaka, kukamilisha ukarabati wa maeneo yaliyobaki katika eneo la Makutupora – Manyoni na Kitaraka – Malongwe –

**Inaendelea Uk. 3**

# WIZARA YAPITISHIWA TRILIONI 1.113 KUENDELEZA SGR



Inatoka Uk. 2

Igalula na kugharamia huduma za ushauri wa kitaalamu katika utekelezaji wa miradi ya ukarabati wa miundombinu ya reli iliyopo inayogharamiwa kwa fedha za Benki ya Dunia.

Waziri Mbarawa amelieleza Bunge kuwa Shirika la Reli Tanzania katika mwaka 2023/24, linalenga kusafirisha tani za mizigo 525,000 na abiria wapatao 716,435 kwa upande wa masafa marefu, abiria 696,730 kwa treni ya kisasa toka Dar es Salaam hadi Morogoro na abiria kwa usafiri wa treni ya mjini (Dar es Salaam Commuter Train) ni 4,368,000.

Aidha, Waziri Mbarawa katika hotuba amelitaarifu Bunge utekelezaji wa mpango wa miaka mitano wa Shirika unaohusisha uendelezaji na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa reli ya Standard Gauge, kuinua kiwango cha reli na madaraja yaliyopo kwa kutandika reli nzito 211 zaidi za angalau ratili 80 kwa yadi na kukarabati madaraja kuweza kupitisha tani 18.5 kwa ekseli, kushirikiana na vyombo vya dola pamoja na jamii inayozunguka miundombinu ya reli ili kuzuia uharibifu wa miundombinu ya reli, kukarabati sehemu korofi za miundombinu ya reli na kununua vitendea kazi kwa awamu, kuweka mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma; na kuendeleza maeneo yanayomilikiwa na TRC ili kuongeza vyanzo vya mapato ya Shirika.

Wakati wa uwasilishaji wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukiz baadhi ya wabunge walipata nafasi ya kuuliza maswali, kutoa ushauri na pongezi kwa kazi inayofanywa ya usimamizi mzuri wa mradi wa ujenzi wa SGR.

“Nampongeza Mhe. Rais, kwasababu kazi ya SGR inaendelea, lakini pia nimpongeze Mkurugenzi Mkuu kwani anafanya kazi sana, kaka yangu Kadogosa fanya kazi Mungu akutie Nguvu sisi tuko nyuma yako” alisema Mhe. Jacquiline Msongozi



# UFAFANUZI KUHUSU KUCHELEWA KUANZA HUDUMA ZA SGR KWA KUTUMIA TRENI YA UMEME



Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa akitoa ufafanuzi kuhusu kuchelewa kuanza kwa majaribio ya treni ya abira katika reli ya kiwango cha kimataifa - SGR, Dodoma Mei 2023.

**Na Mwandishi wetu**

Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Bwana Gerson Msigwa ametoa ufafanuzi kuhusu kuchelewa kuanza utoaji wa huduma za usafiri wa treni za umeme zitakazotembea katika reli ya kiwango cha kimataifa (SGR), Mei 2023.

Bwana Msigwa ameeleza kuwa kuchelewa kuanza kwa huduma kwa kutumia treni ya umeme kulitokana na kutokamilika kwa matengenezo ya vichwa viwili vya kuvuta treni kwa wakati kutokana na sababu za kimsingi na kupelekea majaribio ambayo yalitarajiwa kuanza Mei, 2023 kusogezwa mbele mpaka Julai, 2023.

"Hatuwezi kuendesha treni bila vichwa, baada ya kuvunjika mkataba kati ya TRC na kampuni ya Eurowagon ya nchini Uturuki mkataba wa matengenezo ulihamishiwa kampuni ya Lueckermier Transport and Logistic GMBH ya nchini Ujerumani, kumekuwa na changamoto ya utengenezaji wa vichwa kutokana na shida ya upatikanaji wa vipuri vinavyotumika katika ukamilishaji wa vichwa vya treni kwasababu ya ugonjwa wa UVIKO19 na vita vya Urusi na Ukraine ambavyo vimesababisha kuharibika kwa uchumi Duniani, hizo ni sababu za msingi zilizopelekea ucheleweshaji huo" Amesema Msigwa.

Bwana Msigwa aliendelea kusema kuwa kichwa cha kwanza cha treni kati ya vichwa viwili vinayvotengenezwa nchini Ujerumani na kampuni ya Lueckermeier Transport and Logistic GMBH kitawasili mwezi Julai mwaka huu na kuwezesha shughuli za majaribio ya treni hizo kuanza.

Aidha, Msemaji Mkuu ameongeza kuwa baada ya kupokea Mabehewa 14 Kati ya 59 kutoka kampuni ya Hyundai Rotem ya Nchini Korea Oktoba, 2022 na Mabehewa sita (6) kati ya thelathini(30) yatakayowasili hivi karibuni ambayo yamekarabatiwa na kufikia kwenye ubora wa kiwango cha zaidi ya asilimia 85 yatawezesha kuanza kwa shughuli za uendeshaji haraka.

"Watanzania msiwe na wasiwasi majaribio ya treni yataanza kama tulivyosema mwezi wa Saba mwaka huu baada ya kichwa cha treni kufika na baadaye kuanza kutoa huduma rasmi " Alisema Msigwa.

Bwana Msigwa amesema Serikali inatekeleza mradi wa SGR kwa awamu mbili, awamu ya kwanza ya utekelezaji huo ni ujenzi wa SGR kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na awamu ya pili ya utekelezaji ni kutoka Tabora hadi Kigoma.



Baadhi ya wanahabari wakifuatilia taarifa ya Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa wakati wa mkutano wa wanahabari jijini Dodoma, Mei 2023,



Muonekano wa nje wa mabehewa ya SGR ya ghorofa yanayotarajiwa kuwasili nchini Tanzania mwezi Julai 2023.

# MAANDALIZI YA JIWE LA MSINGI TABORA - KIGOMA



Muonekano wa eneo itakapofanyika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi mradi wa SGR awamu ya pili Tabora - Kigoma likiwa katika maandalizi Katosho mkoani Kigoma, Mei 2023.



Baadhi ya viongozi wa TRC wakiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dkt. Batilda Buriani (kati) mara baada ya kumaliza kikao kwaajili ya maandalaizi ya hafla ya uwekaji jiwe la msingi la mradi wa SGR Tabora Kigoma, Mei 2023.



Timu ya maandalizi kutoka TRC Kwaajili ya hafla ya uwekaji jiwe la msingi la mradi wa SGR pamoja na uongozi wa mkoa wa Kigoma wakikagua eneo litakapofanyika hafla ya uwekaji jiwe la msingi eneo la Katosho mkoani Kigoma, Mei 2023.



Baadhi ya viongozi wa TRC wakiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Urambo, Kenani Kihongosi (kati) mara baada ya kumaliza kikao kwaajili ya maandalaizi ya hafla ya uwekaji jiwe la msingi la mradi wa SGR Tabora Kigoma, Mei 2023.



Baadhi ya viongozi wa TRC wakiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Dinah Mathamani (wa tano kushoto) mara baada ya kumaliza kikao kwaajili ya maandalaizi ya hafla ya uwekaji jiwe la msingi la mradi wa SGR Tabora Kigoma, Mei 2023.




Muonekano wa nje wa mabehewa ya SGR ya ghorofa yakiwa katika Bandari ya Mukran nchini Ujerumani kabla ya kuanza Safari kuja nchini Tanzania.




Mabehewa ya ghorofa kwaajili ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR yakipakiwa ndani ya Meli katika Bandari ya Mukran nchini Ujerumani kwaajili ya kuanza Safari kuja nchini Tanzania.



Muonekano wa ndani wa mabehewa ya ghorofa kwaajili ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR.



Mabehewa ya kisasa ya ghorofa kwaajili ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR yakiwa ndani ya Meli katika Bandari ya Mukran nchini Ujerumani kwaajili ya kuanza Safari kuja nchini Tanzania.



Kazi ya kupakia mabehewa ya kisasa ya ghorofa kwaajili ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR ikiendelea katika Bandari ya Mukran nchini Ujerumani kwaajili ya kuanza Safari kuja nchini Tanzania.

# MAANDALIZI UWEKAJI JIWE LA MSINGI TABORA - KIGOMA YAIVA



**Na Mwandishi Wetu**

Shirika la Reli Tanzania – TRC limeanza maandalizi ya uwekaji jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa – SGR awamu ya pili Tabora – Kigoma linalotarajiwa kuwekwa mwezi Julai 2023.

Viongozi na timu ya wataalamu TRC wamefanya ziara mkoani Tabora na Kigoma kuonana na viongozi wa maeneo ambayo reli ya SGR inapita kwaajili ya kushirikiana katika kukamilisha hafla ya uwekaji jiwe la msingi na kujadili masuala kadhaa ikiwemo ulinzi na usalama wa mradi. Mradi unatarajiwa kupita katika wilaya za Uvinza, Kigoma na Urambo ukiwa na jumla ya kilomita 506.

Meneja mradi wa SGR Tabora – Kigoma Mhandisi Walace Isaya amesema kuwa awamu ya kwanza iko katika utekelezaji, hii ni awamu ya pili ya mradi na ina jumla ya kilomita 506, kilomita 411 za njia kuu na kilomita 95 za mapishano. Ujenzi uko katika hatua za awali na mkandarasi yuko eneo la kazi kuangalia maeneo ya ujenzi wa reli na makambi ya mradi ambapo Shirika tayari limekabidhi maeneo matatu (Nguruka, Uvinza na Urambo) kwaajili ya ujenzi wa kambi ikiwemo kambi kubwa ya mradi eneo la Uvinza kwaajili ya ujenzi na ofisi za mkandarasi, msimamizi wa mradi na TRC .

Aidha, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma Bwana Albert Msovela, ameeleza baadhi ya faida za mradi wa SGR pindi utakapokamilika kwani mkoa wa Kigoma una fursa nyingi za kiuchumi kutokana na uwepo wa Bandari na hitaji kubwa la nchi jirani za Congo, Rwanda na Burundi kusafirisha mizigo kupitia mkoa wa Kigoma.

“Kuja kwa reli ya SGR kunakuja kufungua uchumi wa wilaya zetu zote na ukinzingatia kwamba mkoa wetu unapakana na nchi jirani za Congo, Rwanda na Burundi hivyo usafirishaji wa mizigio utakwenda kuimarika kwasababu sasa hivi tunatumia barabara kwa kiasi kikubwa hii itafungua uchumi wa mkoa” alisema Katibu Tawala mkoa wa Kigoma.

Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Bwana Salumu Kali amesema kuwa “Sisi kwetu tunatoa shukurani kubwa kwa Mhe. Rais, nitahakikisha ulinzi wa vifaa na malighafi zote zinazotumika katika mradi ikiwemo mafuta, nondo, saruji na mitambo mimi mkuu wa Wilaya na kamati ya ulinzi tutahakikisha hakuna kitu kinadokolewa”

Tarehe 20 Disemba 2022 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alishuhudia utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa SGR Tabora – Kigoma ikiwa ni ukamilishaji wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa kutoka Dar es Salaam kuelekea Mwanza na Kigoma.

# ZOEZI LA FIDIA LAENDELEA MKOANI TABORA



Zoezi la fidia likiendelea kwa wananchi waliotwaliwa maeneo yao kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR katika ofisi ya Serikali ya mtaawa ItuluWilaya ya Tabora, Mei 2023.

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania - TRC linaendelea na zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi waliotwaliwa maeneo kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha tatu Makutupora - Tabora lililoanza katika mtaa wa Itulu katika kata ya Ndevelwa wilaya ya Tabora Manispaa mkoani Tabora Mei, 2023.

Afisa Ardhi kutoka TRC Bw. Sweetbert Misango alisema kuwa zoezi hilo ni kwaajili ya wananchi ambao maeneo yao yamepitiwa na njia kuu ya reli ya kisasa katika mradi wa ujenzi wa SGR.

“Maeneo mengi ambayo yametwaliwa yameshafanyiwa uthamini hivyo malipo haya ni kwaajili ya njia kuu, kwa maeneo mengine bado mchakato wa malipo unaendelea ili wananchi wote wakabidhiwe stahiki zao” alisema Bw. Misango.

Mtendaji wa serikali ya mtaa ya Itulu Bw. Bariki Kaponda ameeleza kuwa wananchi wamekua wakisubiri malipo hayo kwa hamu ili kupisha ujenzi ambao utaleta manufaa katika mkoa wa Tabora na nchi kwa ujumla.

“Mradi huu ni wetu sote na serikali inafanya vyema kulipa fidia na kufanya wananchi waweze kuhamia maeneo mengine kwa amani” alisema Bw. Kaponda.

Naye Mwananchi kutoka katika mtaa wa Itulu mkoani Tabora ndugu Mohamedi Pandauyaga alishukuru sana serikali kupitia TRC kwa kuendeleza uhusiano mzuri kwa wananchi katika maeneo yote yaliyotwaliwa na kuzidi kutoa elimu juu ya kuwekeza katika masuala ya maendeleo na kujenga makazi mazuri kwa kufuata mipango miji katika maeneo mapya.

Kipande cha tatu cha mradi wa ujenzi wa SGR Makutupora Tabora chenye jumla ya kilometa 368 hadi sasa kimefikia asilimia 7.57 ambapo ujenzi bado unaendelea katika maeneo mbalimbali yakiwemo eneo la kambi pamoja na njia kuu ya reli ya kisasa.

# WANANCHI MKOANI TABORA WAENDELEA KUTOA USHIRIKIANO KATIKA UTWAAJI ARDHI



Maafisa wa Shirika la Reli Tanzania wakishirikiana na Mthamini kutoka Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Bi. Joyce Mrema (wa pili kulia) kuhakiki taarifa za uthamini kabla ya kuanza zoezi la kuhamisha makaburi ili kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Makutupora - Tabora katika kijiji cha Malongwe wilaya ya Uyui mkoani Tabora, Mei 2023



Afisa wa masuala ya kijamii kutoka Shirika la Reli Tanzania Bi. Grace Mdoe (kushoto) akichukua taarifa za makaburi kutoka kwa wasimamizi wakati wa zoezi la utwaaji ardhi ili kupisha mradi wa SGR Makutupora - Tabora katika kijiji cha Igalula mkoani Tabora, Mei 2023

**Na Mwandishi wetu**

Wananchi waliotwaliwa maeneo yao kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa – SGR kipande cha Makutupora – Tabora waendelea kutoa ushirikiano kwa Shirika la Reli Tanzania – TRC katika zoezi la utwaaji ardhi katika wilaya ya Uyui mkoani Tabora, Mei 2023.

Shirika la Reli Tanzania linaendelea na zoezi la utwaaji ardhi ili kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha Makutupora – Tabora chenye jumla ya urefu wa kilomita 368, inayojumuisha kilomita 294 za njia kuu na kilomita 74 za njia ya kupishana ambao ujenzi wake umefika asilimia saba (7%).

Shirika limekamilisha uthamini kwa urefu wa kilomita 284 kati ya 294 za njia kuu kwaajili ya kuendelea na taratibu za malipo ili kumkabidhi eneo Mkandarasi kampuni ya Yapi Merkezi kutoka Uturuki kwaajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi wa makaravati, tuta, kambi za ujenzi na vituo.

Zoezi la utwaaji ardhi kwa kuhamisha makaburi yaliyopitiwa na mradi linaendelea mkoani Tabora katika vijiji vya Igalula, Goweko, Karangasi na Tura vilivyopo katika wilaya ya Uyui ambapo zaidi ya makaburi 700 yanaendelea kuhamishwa ili kupisha mradi wa SGR.

Uhamishaji wa makaburi unafanyika kwa kufuata taratibu za kiafya na zoezi linasimamiwa na ofisi ya Mganga wa Wilaya husika ili kuhakikisha hakuna madhara ya kiafya kwa wananchi wakati wa zoezi la kuhamisha makaburi.

Kabla ya kuanza zoezi la kuhamisha makaburi wananchi katika vijiji vyote walipatiwa elimu ya uelewa kuhusu zoezi la uhamishaji makaburi katika mikutano iliyofanyika katika vijiji kwa nyakati tofauti ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Uyui Bwana Zakaria Mwansasu.

Mwananchi kutoka kijiji cha Igalula mkoani Tabora Bwana Mtuga Saidi ameeleza kuwa amefurahishwa na ushirikiano ulioonеshwa na wataalamu kutoka TRC, Maafisa afya Wilaya ya Uyui, Viongozi na wananchi wa kijiji cha Igalula katika zoezi la kuhamisha makaburi ya wapendwa wao kwakuwa taratibu zote zimefuatwa katika zoezi hilo.

Zoezi la utwaaji ardhi hufuatiwa na ulipaji wa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yamepitiwa na mradi kwa kuzingatia thamani ya ardhi na mali zisizohamishika katika eneo husika. Aidha, Mkandarasi anaweza kukabidhiwa maeneo yaliyo wazi kwa ridhaa ya mmiliki ili aweze kuendelea na kazi huku mwananchi akisubiri malipo ya fidia. Hatua zote hufuata Sheria na taratibu za utwaaji adhri bila kuathiri mmiliki wa eneo lililotwaliwa.




BODI YA WAHARIRI

MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk, MHARIRI MSAIDIZI/MSANIFU | Sami Omary

HABARI | Hemed Mohamed, Mariam Katunge MAKALA | Aziza Charles, Amina Juma, Athumani Iddy

PICHA | Musa Kadiko, Hassan Mbonde, Augustino Bulegea